



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**MUHTASARI WA PATO LA TAIFA
(APRILI - JUNI) ROBO YA PILI 2021,
MWAKA WA KIZIO 2015**



**Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Wizara ya Fedha na Mipango
Oktoba 2021**

Yaliyomo

Majedwali	3
Orodha ya Vielelezo	4
Viambatisho.....	5
1.0 Utangulizi	6
1.1. Uchumi wa Dunia.....	6
1.2. Nchi Zilizo Kusini Mwa Jangwa la Sahara	6
1.3. Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.....	7
1.4. Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.....	8
1.5. Ukuaji wa Uchumi Nchini Tanzania	9
1.5.1 Pato la Taifa, Robo ya Pili 2021	9
1.5.2 Mchango katika Pato la Taifa, Robo ya Pili Mwaka 2021	9
1.5.3 Ukuaji wa Shughuli za Uchumi, Robo ya Pili ya Mwaka 2021	10
1.5.4 Mchango katika Kiwango cha Ukuaji, Robo ya Pili Mwaka 2021	11
2.0 Ukuaji wa Uchumi Kisekta	11
2.1 Kilimo, Misitu na Uvuvi	11
2.1.1 Mazao	11
2.1.2 Mifugo	12
2.1.3 Misitu.....	12
2.1.4 Uvuvi	13
2.2 Uchimbaji Madini na Mawe.....	13
2.3 Uzalishaji Viwandani	14
2.4 Umembe	14
2.5 Maji	15
2.6 Ujenzi	15
2.7 Biashara na Matengenezo.....	16
2.8 Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo	16
2.9 Malazi na Huduma za Chakula	17
2.10 Habari na Mawasiliano.....	17
2.11 Fedha na Bima.....	18
2.12 Upangishaji Majengo	18
2.13 Shughuli za Kitaalam, Ufundu na Sayansi.....	19
2.14 Huduma Zinazohusiana na Utawala.....	19
2.15 Utawala na Ulinzi	19
2.16 Elimu	20
2.17 Afya ya Binadamu.....	20
2.18 Sanaa na Burudani	20
2.19 Huduma Nyingine za Jamii	21
2.20 Shughuli za Kaya Katika Kuajiri.....	21
3.0 Hitimisho	21

Majedwali

Jedwali Na. 1: Uzalishaji wa Madini, Robo ya Pili Mwaka 2016 – 2021.....14

Jedwali Na. 2: Viashiria vya Huduma za Mawasiliano, Robo ya Pili Mwaka 2017 - 202117

Orodha ya Vielelezo

Kielelezo Na. 1: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za SADC, Robo ya Pili 2020 na 20218
Kielelezo Na 2: Ukuaji wa Uchumi Miongoni mwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Robo ya Pili Mwaka 2016 - 20218
Kielelezo Na. 3: Kiwango cha Ukuaji wa Pato la Taifa, Robo ya Pili Mwaka 2014 - 20219
Kielelezo Na. 4: Mchango katika Pato la Taifa, Bei za Miaka Inayohusika.....10
Kielelezo Na. 5: Viwango vya Ukuaji wa Shughuli za Uchumi, Robo ya Pili Mwaka 202110
Kielelezo Na. 6: Uzalishaji wa Baadhi ya Mazao, Robo ya Pili Mwaka 2020 and 202112
Kielelezo Na. 7: Uzalishaji Maji (Mita za Ujazi Milioni) Robo ya Pili, 2016 - 202115
Kielelezo Na. 9: Jumla ya Mikopo na Amana (Sh. Trillioni), Robo ya Pili Mwaka 2016 - 202118

Viambatisho

Kiambatisho Na. 1: Pato la Taifa kwa Shughuli za kiuchumi kwa Bei za Mwaka 2015 – Sh. Milioni	22
Kiambatisho Na. 2: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za mwaka 2015 – Asilimia	24
Kiambatisho Na. 3: Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za Soko (Bei za Miaka inayohusika) – Sh. Milioni	26
Kiambatisho Na. 4: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Taifa kwa Bei za Soko (Bei za miaka inayohusika) - Asilimia	28

1.0 Utangulizi

Taarifa za Pato la Taifa kwa robo mwaka ni kiashiria chenye taarifa za kina na kinachoaminika kwa ajili ya kutathmini mabadiliko ya kiuchumi katika vipindi vifupi vifupi na pia kuwezesha kutayarisha sera za kiuchumi kwa wakati muafaka katika Nchi.

1.1. Uchumi wa Dunia

Katika mwaka 2021, uchumi wa Dunia unatarajiwa kukua kwa kiwango cha asilimia 6.0 baada ya kufanya mapitio katika mwezi Juni 2021 ambapo ukuaji umebaki kama ilivyokuwa imekadiriwa hapo awali. Kiwango hiki kinalinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 3.3 mwaka 2020. Hata hivyo, ukuaji wa uchumi katika nchi zilizoendelea umefanyiwa mapitio ambapo ukuaji wake umeongezeka kwa pointi za asilimia 0.5 wakati uchumi wa nchi zenyne masoko yanayochipukia na nchi zinazoendelea umepungua kwa pointi za asilimia 0.4 tofauti hiyo ikisababishwa na upatikanaji na pia utumiaji wa chanjo dhidi ya UVIKO-19 na upatikanaji wa misaada ya kifedha kwa ajili ya kukabiliana na athari za UVIKO-19 kwa ajili ya kuwa na uchumi jumuifu. Benki Kuu za nchi mbalimbali zinashauriwa kuendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa bei za bidhaa na huduma kwa ajili ya kuepuka kutumia sera za fedha za kupunguza mzunguko wa fedha katika uchumi hadi hapo changamoto za mabadiliko ya bei zitakapokuwa hazina athari katika uchumi. Mwenendo mdogo wa kutumia chanjo dhidi ya UVIKO-19 Duniani kuliko ilivyotarajiwa unaweza kusababisha mlipuko wa wimbi jingine na hivyo kuongeza zaidi athari za UVIKO-19 kwenye upatikanaji wa fedha kutoka nje na ambapo kasi ya ukuaji wa uchumi itapungua kuliko ilivyotarajiwa. Juhudi za pamoja zinatakiwa zifanyike kati ya Mashirika ya Kimataifa na sera za ndani na za nje za nchi mbalimbali katika kupatihana na kusambaza chanjo dhidi ya UVIKO-19 kwa usawa kwa lengo la kupunguza pengo la ukuaji wa uchumi kati ya mataifa yaliyoendelea na yanayoendelea na hivyo kuimarisha ukuaji wa uchumi wa Dunia.

1.2. Nchi Zilizo Kusini Mwa Jangwa la Sahara


Makadirio ya ukuaji wa uchumi mionganii mwa nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara yaliyokadiriwa Juni 2021 yanaonesha kuongezeka kwa kiwango cha ukuaji wa uchumi kwa asilimia 3.4 kama ilivyokuwa imekadiriwa mwezi Aprili 2021. Kwa sasa uchumi wa Nchi ya Afrika Kusini unakadiriwa kukua kwa kiwango cha asilimia 4.0 mwaka 2021 ikiwa ni ongezeko la pointi za asilimia 0.9 baada ya

mapitio ya Juni 2021 kufanyika ikilinganishwa na ilivyokuwa Aprili 2021. Aidha, makadirio ya ukuaji wa uchumi katika nchi nyingine yameendelea kuwa ya kiwango cha chini kutokana na kutokupatikana kwa chanjo dhidi ya UVIKO-19 na kutokupatikana kwa fedha za kukabiliana na athari ugonjwa huo. Nchi za ukanda huu zinashauriwa kuimarisha upatikanaji wa fedha ili kupunguza athari za UVIKO-19 na hivyo kupunguza kuongezeka zaidi kwa madeni ya nchi. Hatua hizo zikichukuliwa zitaongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na hivyo kuongeza fursa za kutengeneza ajira mpya katika uchumi.

1.3. Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

Ukanda wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ulishuhudia kupungua kwa kiwango cha ukuaji wa uchumi cha asilimia 7.0 mwaka 2020 kutokana na athari za janga la UVIKO-19. Mwaka 2021, ukuaji wa uchumi katika ukanda huu unatarajiwa kuimarika hadi asilimia 3.2. Nchi za ukanda huu hutegemea kwa kiwango kikubwa mapato ya fedha zitokanazo na Sekta ya Utalii iliyoathirika kwa kiwango kikubwa na kuwa na ukuaji hasi wa asilimia 11.5 mwaka 2020 kutokana na athari za janga la UVIKO-19. Kama Janga la UVIKO-19 likidhibitiwa ipasavyo na biashara ya utalii kurejea kama ilivyokuwa hapo awali, uchumi wa ukanda huu unatarajiwa kurejea katika kiwango cha awali cha ukuaji wa uchumi wa asilimia 6.8 mwaka 2021. Katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2021, viwango vya ukuaji wa uchumi kwa baadhi ya Nchi za ukanda huu uliimarika na kuongezeka kwa kiwango chanya ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2020 ambapo uchumi wa Nchi ya Afrika Kusini uliongezeka kwa asilimia 19.3 ikilinganishwa na kiwango hasi cha asilimia 16.8; uchumi wa Namibia uliongezeka kwa kiwango cha asilimia 1.6 ikilinganishwa na kiwango hasi cha asilimia 11.6; uchumi wa Mauritius uliongezeka kwa asilimia 18.8 ikilinganishwa na kiwango hasi cha asilimia 33.0. Aidha, uchumi wa Msumbiji uliongezeka kwa asilimia 1.9 ikilinganishwa na kiwango hasi cha asilimia 3.5 na uchumi wa Tanzania uliongezeka kwa asilimia 4.3 ikilinganishwa na asilimia 4.0 kipindi kama hicho mwaka 2020.

Kielelezo Na. 1: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za SADC, Robo ya Pili 2020 na 2021




Chanzo: Ofisi za Takwimu za Nchi Husika

1.4. Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ziliendelea kuonesha ukuaji wa uchumi wa kuridhisha na imara ambapo kiwango cha ukuaji kwa mwaka 2019 kilikuwa asilimia 5.0. Aidha, mwaka 2020 uchumi wa Nchi za ukanda huu uliathirika kutohana na athari za Janga la UVIKO-19 na kusababisha kupungua kwa ukuaji wa uchumi kwa kiwango cha asilimia 0.7. Uchumi katika ukanda huu unatarajiwa kukua kwa kiwango cha asilimia 3.0 mwaka 2021. Viwango vya ukuaji unaotarajiwa kwa nchi za ukanda huu ni kama ifuatavyo: Uchumi wa Kenya unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.0, Tanzania asilimai 5.0 na Rwanda asilimia 3.9.

Kielelezo Na. 2: Ukuaji wa Uchumi Mionganini mwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Robo ya Pili Mwaka 2016 - 2021



Chanzo: Ofisi za Takwimu za Nchi Husika

1.5. Ukuaji wa Uchumi Nchini Tanzania

Utayarishaji wa Takwimu za Pato la Taifa robo ya pili (Aprili - Juni) mwaka 2021 umetumia taarifa zilizokusanywa kutoka katika shughuli zote za uchumi nchini. Aidha, utayarishaji umezingatia Mwongozo wa Kimataifa wa Kutayarisha takwimu za Pato la Taifa unaojulikana kama *System of National Accounts 2008*. Taarifa hii ya Pato la Taifa ni imetumia bei za mwaka husika na bei za mwaka wa kizio 2015.

Ofisi ya Taifa ya Takwimu inatekeleza Sera ya Mapitio ya Takwimu za Pato la Taifa. Sera hii ilianza kutumika mwanzoni mwa mwaka 2019 na inaruhusu kuchapisha takwimu zilizofanyiwa mapitio kutokana na upatikanaji wa takwimu mpya za kila robo mwaka na za kila mwaka.

1.5.1 Pato la Taifa, Robo ya Pili 2021

Katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2021, Pato la Taifa katika bei za mwaka husika liliongezeka hadi Shilingi trilioni 39.2 kutoka Shilingi trilioni 37.2 kipindi kama hicho mwaka 2020. Aidha, Pato la Taifa katika bei za mwaka 2015 liliongezeka hadi Shilingi trilioni 33.4 katika robo ya pili ya mwaka 2021 kutoka Shilingi trilioni 32.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2020 sawa na kiwango cha ukuaji cha asilimia 4.3.


Robo Mwaka	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021
1	8.5	2.9	9.7	4.9	7.5	6.2	5.9	5.0
2	8.7	6.7	8.2	6.7	6.0	7.4	4.0	4.3
3	4.7	7.6	6.6	5.0	7.2	8.1	4.4	
4	5.1	7.4	3.4	10.2	7.1	6.4	4.8	
Mwaka	6.8	6.2	7.0	6.7	7.0	7.0	4.8	

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

1.5.2 Mchango katika Pato la Taifa, Robo ya Pili Mwaka 2021

Shughuli za Huduma ziliikuwa na mchango mkubwa zaidi katika Pato la Taifa wa asilimia 38.9 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2021, zikifuatiwa na shughuli za Msingi (asilimia 36.9) na shughuli za Kati (asilimia 24.2). Ukokotoajia wa Mchango katika Pato la Taifa umetayarishwa kabla ya kujumuisha kodi.

Kielelezo Na. 3: Mchango katika Pato la Taifa, Bei za Miaka Inayohusika




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

1.5.3 Ukuaji wa Shughuli za Uchumi, Robo ya Pili ya Mwaka 2021

Katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2021, Shughuli ya Habari na Mawasiliano ilikuwa na kiwango cha juu zaidi cha ukuaji wa asilimia 12.3 ikifuatiwa na Uzalishaji Umeme (asilimia 12.1); Huduma Nyingine za jamii zinazojumuisha Sanaa na Burudani; na shughuli za Kaya katika Kuajiri (asilimia 10.8); Malazi na Huduma za Chakula (asilimia 10.1); Usambazaji Maji (asilimia 8.4) na Uchimbaji madini na mawe (asilimia 7.3).

Kielelezo Na. 4: Viwango vya Ukuaji wa Shughuli za Uchumi, Robo ya Pili Mwaka 2021



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

1.5.4 Mchango katika Kiwango cha Ukuaji, Robo ya Pili Mwaka 2021

Shughuli zote za uchumi zilizofanyika katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2021 zilichangia ukuaji wa uchumi kwa kiwango cha asilimia 4.3 ikilinganishwa na asilimia 4.0 kipindi kama hicho mwaka 2020. Shughuli za uchumi zilizokuwa na mchango mkubwa katika ukuaji huo ziliwu ni pamoja na: Kilimo (asilimia 13.0), Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo (asilimia 8.4) Biashara na Matengenezo (asilimia 8.1), Chimbaji Madini na Mawe (asilimia 7.6); Uzalishaji Viwandani (asilimia 7.6) Ujenzi (asilimia 7.1) na Habari na Mawasiliano (asilimia 5.2).

2.0 Ukuaji wa Uchumi Kisekta

2.1 Kilimo, Misitu na Uvuvi


Shughuli hii inahusika na uvunaji wa rasilimali za asili za mboga za majani na wanyama zinazojumuisha mazao ya kupandwa, ufugaji na uzalishaji wa wanyama, uvunaji wa miti na mimea mingine, wanyama au bidhaa za wanyama kutoka katika mashamba ya ufugaji au mazingira ya asili. Shughuli za Kilimo, Misitu na Uvuvi iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 2.2 katika robo ya pili ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 4.2 kipindi kama hicho mwaka 2020.

2.1.1 Mazao

Mazao makuu yaliyojumuishwa ni pamoja na mahindi, mpunga, ulezi/mtama, nafaka nyingine, mihogo, viazi mviringo, viazi vitamu, maharagwe, mikunde, mbegu za mafuta, mboga mboga, ndizi, matunda mengine, karanga, kahawa, pamba, chai, tumbaku na mazao mengine ya chakula na biashara.

Shughuli hii iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 2.2 katika robo ya pili ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 4.5 kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji ulichangiwa na upatikanaji wa mvua za kutosha katika maeneo ya uzalishaji wakati wa kipindi cha mvua za masika.

Kielelezo Na. 5: Uzalishaji wa Baadhi ya Mazao, Robo ya Pili Mwaka 2020 and 2021



Chanzo: Wizara ya Kilimo

Katika kipindi cha robo ya pili, mazao yaliyokuwa na mchango mkubwa wa ukuaji yalikuwa ni pamoja na mahindi yaliyoongezeka kwa asilimia 2.0 kutoka Tani milioni 3.224 mwaka 2020 hadi Tani milioni 3.290 mwaka 2021; Maharage na Mikunde yaliongezeka kwa asilimia 7.9 kutoka Tani elfu 119 mwaka 2020 hadi Tani elfu 129 mwaka 2021; Mtama uliovunwa uliongezeka kwa asilimia 23.3 kutoka tani elfu 93 mwaka 2020 hadi tani elfu 115 mwaka 2021; Viazi mviringo viliongezeka kwa asilimia 2.9 kutoka Tani elfu 87 mwaka 2020 hadi Tani elfu 89 mwaka 2021. Mpunga uliongezeka kwa asilimia 5.4 kutoka Tani elfu 1,824 mwaka 2020 hadi Tani elfu 1,922 kipindi kama hicho mwaka 2021.

2.1.2 Mifugo

Shughuli hii inahusika na ufgajji ng'ombe wa asili na wa kisasa, mbuzi; kondoo; punda, farasi; nguruwe, sungura, kuku wa kienyeji na kisasa; na ndege wa aina nyingine.

Katika kipindi cha robo ya pili mwaka 2021, uzalishaji wa mifugo uliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.0 sawa na ukuaji wa kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji huu ulichangiwa na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa za mifugo kutokana na kuongezeka kwa wastani wa pato la mwananchi, ukuaji wa miji pamoja na kuongezeka kwa uelewa wa wananchi juu ya umuhimu wa lishe bora.

2.1.3 Misitu

Shughuli hii inahusisha uzalishaji na uvunaji wa mazao ya misitu kama vile magogo, mkaa, kuni, matawi ya mti, na bidhaa nyingine zisizo za miti kama asali na nta.

Shughuli ya misitu ilikuwa na kiwango kidogo cha ukuaji wa asilimia 0.8 katika robo ya pili mwaka 2021 ikilinganishwa ana asilimia 5.1 kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji wa shughuli hii ulichangiwa na hatua za Serikali za kusimamia uvunaji endelevu wa mazao ya misitu.

2.1.4 Uvuvi

Shughuli ya uvuvi inahusika na uvunaji wa rasilimali za uvuvi katika maji ya bahari na vyanzo vingine vya maji baridi.

Shughuli ya uvuvi iliendelea kupungua na kuwa na kiwango hasi cha ukuaji wa asilimia 6.0 katika robo ya pili ya mwaka 2021 ikilinganishwa na kiwango hasi cha asilimia 2.1 kipindi kama hich mwaka 2020. Kasi ya kupungua kwa ukuaji ilisababishwa na kendelea kupungua kwa mazao ya uvuvi katika kipindi hicho.

2.2 Uchimbaji Madini na Mawe

Shughuli ya uchimbaji wa Madini na Mawe inahusisha madini yabisi kama vile makaa ya mawe, vimiminika (petroli) au gesi (gesi asilia). Uchimbaji wa madini na mawe hufanyika chini ya ardhi, ukusanyaji juu ya ardhi au kwenye visima. Pia inajumuisha shughuli za ziada zinazolenga kutayarisha madini kwa ajili ya kuuzwa, kwa mfano, kusaga, kusafisha na kukausha. Shughuli hizi mara nyingi zinafanywa na vitengo ambavyo vinavuna rasilimali za madini / au nyingine zilizopo karibu na migodi.

Shughuli ya uchimbaji wa madini na mawe imegawanyika katika maeneo makuu manne ambavyo ni:

- 1) Madini ya makaa ya mawe;
- 2) Petroli na gesi asilia;
- 3) Uchimbaji wa madini ya chuma; na
- 4) Madini ya kokoto na mawe.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya uchimbaji wa madini na mawe iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 7.3 katika robo ya pili ya mwaka 2021 ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 8.7 kipindi kama hicho mwaka 2020. Kiwango cha ukuaji kilisababishwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa madini ya dhahabu ambayo ndiyo yenye mchango mkubwa zaidi katika shughuli ya uchimbaji madini na mawe.

Katika kipindi hicho, uzalishaji wa dhahabu uliongezeka hadi kilogramu 15,359.30 mwaka 2021 kutoka kilogramu 14,512.43 kipindi kama hicho mwaka 2020.

Jedwali 2: Uzalishaji wa Madini, Robo ya Pili Mwaka 2016 – 2021

Madini	Kipimo	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Dhahabu	Kg	11,577	9,889	9,539	10,683	14,512	15,359
Makaa ya							
Mawe	Tani	64,291	128,685	160,367	181,236	148,869	190,593
Jasi	Tani	41,402	29,928	49,622	33,029	95,539	124115
Chumvi	Tani	20,827	27,157	44,296	30,268	9,311	15,949
Almasi	Karati	58,068	65,076	81,860	97,601	10,953	5,126

Chanzo: Wizara ya Madini

2.3 Uzalishaji Viwandani

Shughuli ya uzalishaji viwandani inahusisha uchakataji wa bidhaa kutoka katika hali yake ya kawaida na kuzalisha bidhaa za aina nyingine ambazo zinaweza kutumika moja kwa moja na mlaji wa mwisho au kutumika kuzalisha bidhaa nyingine. Bidhaa zinazoweza kuchakatwa ni pamoja na bidhaa za kilimo, misitu, uvuvi, madini na bidhaa nyingine za viwandani.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya Uzalishaji Viwandani iliongezeka zaidi hadi asilimia 4.3 katika robo ya pili ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 4.0 kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji huu ulichangiwa na ongezeko la uzalishaji wa bidhaa za viwandani.

2.4 Umeme

Shughuli hii inahusika na uzalishaji na usambazaji wa umeme na gesi asilia, kupitia miundombinu ya kudumu ya waya na mabomba. Uzalishaji wa umeme ni kutoka katika vyanzo vya maji, mafuta na gesi. Pia inahusika na shughuli za usambazaji na ugawaji wa umeme. Vyanzo vikuu vya takwimu za uzalishaji wa umeme ni kutoka katika makampuni ya uzalishaji wa umeme.

Ukuaji wa shughuli ya uzalishaji wa umeme hutegemea kiasi cha umeme kilichozaishwa na kusambazwa kwa wateja mbalimbali wa nishati ya umeme. Katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2021, umeme uliosambazwa kwa wateja uliongezeka hadi kWh milioni 1,764 kutoka kWh 1,589 kipindi kama hicho mwaka 2020. Shughuli ya uzalishaji umeme iliongezeka kwa kiwango kikubwa cha asilimia

12.1 katika robo ya pili ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 3.3 kipindi kama hicho mwaka 2020.


2.5 Maji

Shughuli hii inahusika na kukusanya na kusafisha maji kwa ajili ya ugavi wa maji, kusafisha maji ya bahari kwa kuondoa chumvi ili kuweza kuzalisha maji ya kutumia kama bidhaa kuu na kukusanya maji moja kwa moja kutoka katika visima kwa ajili ya matumizi ya makampuni ya maji au matumizi binafsi katika kilimo au kaya. Aidha, shughuli hii pia inahusika na ukusanyaji wa maji taka.

Kiashiria cha kuongezeka kwa kiwango cha ukuaji wa shughuli ya usambazaji maji ni kiasi cha maji kilichozalishwa. Katika robo ya pili ya mwaka 2021, kiasi cha maji kilichozalishwa kiliongezeka hadi mita za ujazo milioni 81.6 kutoka mita za ujazo milioni 74.7 kipindi kama hicho mwaka 2020.

Shughuli ya usambazaji maji ilikua hadi asilimia 8.4 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2021 kutoka asilimia 4.6 kipindi kama hicho mwaka 2020. Sababu zilizochangia ongezeko hilo ni pamoja na kuendelea kuboreshwa kwa miundombinu ya uzalishaji maji kwa lengo la kuongeza uwezo wa uzalishaji na kuendelea kuzalisha maji zaidi ili kukidhi mahitaji ya maji ambayo yanaendana na ongezeko la idadi ya watu hususani katika maeneo ya mijini.

Kielelezo Na. 6: Uzalishaji Maji (Mita za Ujazi Milioni) Robo ya Pili, 2016 - 2021



Chanzo: Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji

2.6 Ujenzi

Shughuli hii inajumuisha ujenzi wa aina zote na shughuli maalum za ujenzi kwa ajili ya majengo na kazi za uhandisi. Shughuli hii inajumuisha pia ujenzi mpya,

ukarabati, kufanya mabadiliko makubwa kwenye majengo na ujenzi wa miundombinu.

Ujenzi wa aina zote unajumuisha ujenzi wa nyumba nzima, majengo ya biashara/ofisi, maduka na majengo mengine ya umma na miundombinu ya mashambani. Ujenzi pia unajumuisha ujenzi wa barabara, madaraja, reli, viwanja vya ndege, bandari na miundombinu ya maji, mifumo ya umwagiliaji, mifumo ya majitaka, miundombinu ya viwanda, mabomba na mifumo ya umeme na vituo vya michezo.

Shughuli ya ujenzi iliongezeka kwa kiwango kidogo cha asilimia 1.9 katika robo ya pili ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 12.2 ya kipindi kama hicho mwaka 2020. Tathmini ya ukuaji wa shughuli ya ujenzi hutumia uzalishaji wa bidhaa za ndani ya nchi zinazotumika katika shughuli za ujenzi. Kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa hizo ambazo ni pamoja na chuma zilichangia ukuaji huo.

2.7 Biashara na Matengenezo

Shughuli hii inajumuisha uuzaaji wa jumla na rejareja (uuzaaji wa bidhaa bila ya kufanya mabadiliko) wa aina yoyote ya bidhaa, pamoja na utoaji wa huduma kwa ajili ya uuzaaji wa bidhaa. Pia inahusisha ukarabati wa magari na usimikaji wa mitambo na ukarabati wa bidhaa za binafsi na za nyumbani. Shughuli kuu ni kununua na kuuza bidhaa.

Ukuaji wa shughuli za Biashara na Matengenezo ziliongezeka kwa kiwango kikubwa cha asilimia 4.2 katika robo ya pili ya mwaka 2021 ikilinganishwa na kiwango hasi cha asilimia 0.2 kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji wa shughuli hii ulichangiwa na kuongezeka kwa bidhaa zilizouzwa ikiwa ni pamoja na bidhaa za kilimo.

2.8 Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo

Shughuli hii inahusisha utoaji wa huduma ya usafiri wa abiria au/na mizigo, ikiwa ni kwa ratiba maalum au isiyokuwa na ratiba, kwa njia ya reli, bomba, barabara, maji au anga na shughuli zinazohusiana ikiwa ni pamoja na utunzaji wa mizigo na uhifadhi. Shughuli hii pia inajumuisha kukodisha vifaa vya usafiri na madereva na shughuli za posta na usafirishaji wa vifurushi.

Kasi ya ukuaji wa shughuli ya Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo ilipungua hadi asilimia 4.6 katika robo ya pili ya mwaka 2021 kutoka kiwango cha asilimia 9.5 kipindi kama hicho mwaka 2020. Ongezeko hili lilitokana na idadi ya abiria na mizigo iliyosafirishwa katika kipindi hicho.

2.9 Malazi na Huduma za Chakula

Shughuli hii inajumuisha utoaji huduma ya makazi ya muda mfupi kwa wageni na wasafiri wengine na utoaji wa huduma ya chakula na vinywaji kwa mlaji wa mwisho.

Shughuli ya Malazi na Huduma ya Chakula iliongezeka kwa kiwango kikubwa cha asilimia 10.1 katika robo ya pili ya mwaka 2021 ikilinganishwa na kiwango hasi cha asilimia 15.9 kipindi kama hicho mwaka 2020. Kasi ya ukuaji ilichangiwa na ongezeko kubwa la watalii 143,828 walioingia nchini katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2021 ikilinganishwa na watalii 22,269 walioingia nchini kipindi kama hicho mwaka 2020.

2.10 Habari na Mawasiliano

Shughuli hii inahusika na uchapishaji, upigaji picha za kawaida, picha za video na uzalishaji wa programu za televisheni, kurekodi sauti na kuchapisha muziki, shughuli za programu na utangazaji, kwa mfano, utangazaji wa redio na televisheni, mawasiliano ya simu, programu za kompyuta, ushauri na shughuli zinazohusiana na shughuli za huduma za habari kama vile uchakataji wa taarifa.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya Habari na Mawasiliano iliongezeka hadi asilimia 12.3 katika robo ya pili ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 9.9 katika robo ya pili ya mwaka 2020. Kasi ya ukuaji ilichangiwa na kuongezeka kwa muda wa maongezi, ujumbe mfupi uliotumwa na kuongezeka kwa idadi ya wateja waliopata huduma za fedha kupitia mitandao ya simu pamoja na huduma za utangazaji na huduma za inteneti kwa ujumla.

Jedwali Na. 3: Viashiria vya Huduma za Mawasiliano, Robo ya Pili Mwaka 2017 - 2021

Kiashiria, kwa Robo Mwaka	2017	2018	2019	2020	2021
Muda wa Maongezi (Milioni) uliotumika	12,926.50	15,188.40	16,108.40	19,704.10	21,799.40
Ujumbe Mfupi (Milioni)uliotumwa	19,095.7	23,189.1	25,206.1	35,502.9	35,534.4
Wateja wa Fedha Mitandao ya Simu (000)	20,285.8	20,855.2	22,957.5	29,659.9	33,282.5

Chanzo: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania


Tanbihi: Idadi ya Wateja ni kama ilivyokuwa Mwezi Juni, 2021.

2.11 Fedha na Bima

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma za fedha, bima, pensheni ya hiari, na huduma nyingine za fedha.

Huduma za Fedha na Bima ziliongezeka kwa kiwango cha asilimia 4.0 katika robo ya pili ya mwaka 2021 ikilinganishwa na silimia 3.0 katika robo ya pili ya mwaka 2020. Ukuaji wa shughuli za Fedha na Bima zilichangiwa na kuongezeka kwa asilimia 8.6 kwa amana kutoka shilingi trilioni 23.3 mwaka 2020 hadi shilingi trilioni 25.3 mwaka 2021; ongezeko la asilimia 5.4 la mikopo kutoka shilingi trilioni 19.1 mwaka 2020 hadi shilingi trilioni 20.1 mwaka 2021; na kuongezeka hadi kiwango cha ukuaji wa asilimia 5.2 wa shughuli za Bima mwaka 2021 kutoka asilimia 2.9 kipindi kama hicho mwaka 2020.

Table4: Jumla ya Mikopo na Amana (Sh. Trilioni), Robo ya Pili Mwaka 2016 - 2021



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

2.12 Upangishaji Majengo

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma za kuuza au kununua majengo, kukodisha mali, majengo na pia kutoa huduma nyingine za mali isiyohamishika ikiwa ni pamoja na kupima mali isiyohamishika kama vile viwanja.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya Upangishaji Majengo iliongezeka kwa asilimia 4.6 mwaka 2021 kama ilivyokuwa katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Ongezeko la huduma za malazi hususani katika maeneo ya mjini lilichangia ukuaji wa shughuli hii ya uchumi.

2.13 Shughuli za Kitaalam, Ufundu na Sayansi

Shughuli hii inajumuisha shughuli maalum za kitalaam, kisayansi na kiufundi. Shughuli hizi zinahitaji kiwango cha juu cha mafunzo, pamoja na kupata ujuzi maalum unaotumika kutoa huduma kwa watumiaji. Shughuli hii inahusisha huduma za kisheria na uhasibu; ushauri na usimamizi; usanifu na uhandisi; kupima na uchambuzi wa kitaalam; utafiti wa kisayansi na maendeleo; matangazo na utafiti wa masoko; utaalamu wa aina nyingine wa kisayansi na kiufundi pamoja na shughuli za ugani.

Kasi ya ukauji wa shughuli za Kitaalam, Kisanyansi na Ufundu ilipungua kidogo hadi asilimia 7.6 katika robo ya pili ya mwaka 2021 kutoka asilimia 8.8 kipindi kama hicho mwaka 2020. Ongezeko la huduma za kisheria na uhasibu katika shughuli hii ya uchumi lilichangia ukuaji uliofikiwa.

2.14 Huduma Zinazohusiana na Utawala

Shughuli hii inajumuisha huduma mbalimbali zinazosaidia kufanyika kwa biashara. Shughuli inajumuisha huduma za kukodisha vifaa, ajira, huduma za uwakala wa kampuni za usafiri, huduma za kuongoza watalii, huduma za kuandaa malazi; na huduma nyingine zinazohusiana na usalama na uchunguzi; pamoja na huduma kwenye majengo na uboreshaji wa mazingira.

Kasi ya ukuaji wa Huduma zinazohusiana na Utawala ilipungua kidogo hadi asilimia 7.3 katika robo ya pili ya mwaka 2021 kutoka asilimia 7.9 kipindi kama hicho mwaka 2020. Kuongezeka kwa huduma za uwakala wa usafiri wa watalii ulichangia ukuaji wa shughuli hii.

2.15 Utawala na Ulinzi

Shughuli ya utawala na ulinzi inahusika na kutunga na kutafsiri sheria, kukusanya kodi, ulinzi wa mipaka ya nchi, usalama wa raia na mali zao, huduma za uhamiaji, pamoja na uendeshaji wa serikali kwa ujumla. Aidha, huduma za mifuko ya hifadhi ya jamii ya lazima imejumuishwa katika Utawala na Ulinzi.

Ukuaji wa shughuli ya Utawala na Ulinzi uliimarika zaidi hadi asilimia 4.0 katika robo ya kwanza ya mwaka 2021 kutoka asilima 3.8 kipindi kama hicho mwaka 2020. Ongezeko la matumizi ya fedha za Serikali katika kazi za ulinzi na usalama na utoaji wa huduma za afya na elimu.

2.16 Elimu

Shughuli hii inajumuisha utoaji wa elimu katika ngazi zote, kwa njia ya kuongea au maandishi au kwa njia ya redio na televisheni au njia nyingine za mawasiliano. Inajumuisha elimu inayotolewa na taasisi tofauti katika mfumo wa kawaida wa shule katika ngazi tofauti tofauti pamoja na elimu ya watu wazima na elimu ya kujifunza kusoma na kuandika. Shughuli hii inajumuisha elimu katika sekta ya umma na binafsi.

Shughuli ya Elimu iliongezeka kwa kiwango kikubwa cha asilimia 4.7 katika robo ya pili ya mwaka 2021 ikilinganishwa na kiwango hasi cha asilimia 1.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji wa shughuli hii umetokana na kuongezeka kwa udahili wa wanafunzi katika shule za msingi na sekondari za umma na binafsi ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa matumizi ya Serikali katika utoaji wa elimu bila ada.

2.17 Afya ya Binadamu

Shughuli hii inajumuisha utoaji wa huduma za afya na maendeleo ya jamii. Inajumuisha huduma za afya zinazotolewa na wataalam wa matibabu katika hospitali na vituo vingine, shughuli nyingine za huduma za makazi ambazo zinahusisha shughuli za huduma za afya kwa jamii bila ushirikishwaji wa wataalamu wa huduma za afya.

Shughuli ya utaoji wa huduma za afya iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 4.8 katika robo ya pili ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 5.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2020.

2.18 Sanaa na Burudani

Shughuli hii inajumuisha shughuli mbalimbali zinazotolewa ili kukidhi maslahi mbalimbali ya kitamaduni na utoaji wa burudani kwa umma kwa ujumla. Shughuli hii pia inahusika na burudani za bendi, uendeshaji wa maeneo ya makumbusho, kamari, shughuli za huduma michezo na burudani kwa ujumla.

Shughuli ya Sanaa na Burudani iliongezeka kwa kiwango kikubwa cha asilimia 25.1 katika robo ya pili ya mwaka 2021 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 9.3 kipindi kama hicho mwaka 2020. Ongezeko kubwa la watalii walioingia nchini

katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2021 limechangia kuimarka kwa ukuaji wa shughuli hii ya uchumi.

2.19 Huduma Nyingine za Jamii

Shughuli hii inajumuisha shughuli za mashirika ya uanachama, ukarabati wa vifaa vya kieletroniki na bidhaa za kibinafsi za nyumbani na shughuli mbalimbali za huduma za binafsi ambazo hazijumuishwi kwenye shughuli nyingine.

Kasi ya ukuaji wa shughuli ya Huduma nyingine za Jamii iliendelea kuongezeka hadi asilimai 7.9 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2021 kutoka asilimia 5.4 kipindi kama hicho mwaka 2020. Ongezeko la idadi ya watu katika maeneo ya mjini na mahitaji ya huduma za jamii kumechangia ukuaji wa shughuli hii ya uchumi.

2.20 Shughuli za Kaya Katika Kuajiri

Shughuli za kaya kama mwajiri zinajumuisha wafanyakazi wa ndani kama vile wajakazi, wapishi, wahudumu, wafugaji, watengenezaji wa bustani, wakulima, walini wa mlangoni, madereva wa magari, waangalizi wa watoto, wafundishaji na masekretari. Bidhaa na huduma zinazozalishwa na shughuli hii hutumiwa na kaya inayoajiri.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli za Kaya katika Kuajiri kimeendelea kubaki katika asilimia 3.1 katika robo ya pili ya mwaka 2021 kama ilivyokuwa katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2020. Ukuaji huu unatokana na ukuaji wa idadai ya watu katika maeneo ya mjini.

3.0 Hitimisho

Katika kipindi cha robo ya pili mwaka 2021, Pato Halisi la Taifa liliongezeka kwa kiwango cha asilimia 4.3 kutoka asilimia 4.0 kipindi kama hicho mwaka 2020. Shughuli zilizoongezeka kwa kiwango kikubwa zilikuwa Habari na Mawasiliano (asilimia 12.3); Usambazaji Umeme (asilimia 12.1); Huduma Nyingine za Jamii zikijumuisha Sanaa na Burudani; na shughuli za Kaya katika Kuajiri (asilimia 10.8); Malazi na Huduma ya Chakula (asilimia 10.1); Maji (asilimia 8.4) na Uchimbaji madini na mawe (asilimia 7.3).

Kiambatisho Na. 1: Pato la Taifa kwa Shughuli za kiuchumi kwa Bei za Mwaka 2015 – Sh. Milioni

Mwaka	Robo mwaka	kilimo	Madini na Mawe	Viwanda	Umeme	Maji safi na maji taka	Ujenzi	Biasara na Matengen ezo	Malazi na Hudum a ya Chakula	Uchukuzi na Uhifadhi Mizigo	Habari na Mawasili ano	Fedha na Bima
2012		21,807,030	3,314,742	6,066,989	669,069	358,361	7,578,263	7,371,411	1,343,924	5,710,466	1,266,747	3,444,161
2013		22,408,192	3,464,721	6,292,514	723,608	367,890	9,023,353	7,682,286	1,356,204	6,050,976	1,414,116	3,405,940
2014		23,952,077	3,687,273	6,919,794	815,297	381,760	9,253,082	8,444,243	1,397,782	6,577,706	1,560,064	3,764,113
2015		25,234,560	4,055,619	7,411,672	798,801	390,758	10,446,797	8,747,862	1,421,916	6,929,895	1,681,098	4,189,021
2016		26,436,338	4,356,709	8,213,364	869,262	417,899	11,960,720	9,260,703	1,480,052	7,324,856	1,718,548	4,235,515
2017		28,008,976	4,588,624	8,889,818	877,667	444,660	13,765,005	9,821,248	1,525,619	7,815,845	1,824,471	4,115,393
2018		29,504,198	4,659,195	9,623,501	928,174	477,510	15,655,747	10,396,691	1,604,391	8,736,561	1,989,717	4,094,972
2019		30,802,027	5,485,112	10,184,558	994,879	510,411	17,802,021	10,965,038	1,645,950	9,493,191	2,133,312	4,281,167
